
## KITABU CHA KIADA



Chuo cha Biblia na Ukombozi Moshi, Kilimanjaro, TANZANIA

Chuo cha Biblia na Ukombozi Portland, Maine, AMERIKA

# Elimu ya Mahubiri I

## Maandalizi ya Hotuba na Mahubiri

Utangulizi kwa Elimu ya	
	Mahubiri
	2
Umuhimu wa kuhubiri kwa Nguvu za Roho	
	Mtakatifu.
	6
Mafundisho ya Neno la	
	Mungu

	•••••
	10
Kutoa	
	Hotuba
	13
Wasifu wa	
	Mhubiri
	14
Kuhubiri	
	Kikristo

	2
	1
I. Mambo ya	
kuhubiri	21
II. Njia ya	
kuhubiri	24
III. Malengo ya	
kuhubiri	26
Dhamira na Hoja	27
Kifungu Cha	
	Maandiko.
	32
I. Matuzimi ya kifungu cha	
Maandiko32	

II. Umbile la kifungu cha	
Maandiko	34
III. Kufonyia kazi kifungu cha	
Maandiko36	

## Utangulizi Kwa Elimu Ya Mahubiri I

Elimu ya mahubiri ni sayansi au sanaa ya kidini. Katika darasa hili wanafunzi watapata msaada wa namna ya kuandaa hotuba na kuhubiri. Darasa hili halitakufanya uwe mhubiri; ni Mungu peke yake anayeweza kumfanya mhubiri. Katika darasa hili wanafunzi walioitwa na Mungu watapata msaada wa kujiandaa kwa kazi ya kulihubiri Neno Takatifu.

Utajifunza namna ya kupanga ulivyojifunza kiwe na maana moja au somo. Masomo yaliyomo katika Biblia yana dhamira moja. Dhamira ndilo somo moja la msingi au wazo ambalo litaongoza mahubiri. Kuhutubia kwa dhamira moja ndio **mfumo wa Biblia**. Njia hii inafanya mahubiri yaeleweke kwa urahisi kwa waumini na kupokelewa. Elimu ya mahubiri bora humsaidia mhubiri akae ndani ya ujumbe ambao Mungu amempatia kwa ajili ya watu wake.

#### I. Kuhubiri ni kufanya kitu gani?

#### A. Njia ya Mungu

Kuhubiri ni mawasiliano kwa maneno ya ukweli wa Mungu kwa lengo la kushawishi - kushauri na kuhimiza wanadamu watambue umuhimu wake. Kamusi unaelezea mahubiri kama: *kutangaza au kuweka hadharani injili*.

Kuhubiri kwa hakika siyo kuongea tu kuhusu Biblia, bali ni kupata uamuzi mioyoni mwa wanadamu. Wokovu wa Roho za watu ni moja ya malengo muhimu ya mahubiri. Mahubiri ni njia aliyochagua Mungu ya kuifikia mioyo ya wanadamu. Mungu amechagua kumtumia mwanadamu kumfikishia ujumbe wa Neno lake mwanadamu. Watenda dhambi hawatamuona Mungu kwa hekima ya mwanadamu, bali kwa kupitia mahubiri ya ujumbe wa Neno lake.

I Kor.1:21- Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa.

#### B. Neno la Mungu

1. Katika msitari unaotangulia wa darasa hili (II Tim.4:2), Paulo alimwambia Timoteo **lihubiri Neno**.

Mhubiri anaitwa alitangaze Neno la Mungu. Neno la Mungu ndiyo mamlaka ya mwisho. Mhubiri anapaswa kujibu kila swali kwa kutumia Neno la Mungu; analazimika kutulia katika mamlaka kuu ya Maandiko.

- II Tim.4:2 Lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.
- 2. Neno la Mungu lina nguvu za kuweza kubalisha maisha ya wanadamu na Neno la mahubiri linahitajika ili kupata mabadiliko hayo.

Mawazo ya mwanadamu hayatabadilisha maisha. Ni sharti muhubiri atumie Neno la Mungu kama msingi wa hotuba yake. Upo <u>uhai</u> katika Neno la Mungu.

- Rum.1:16 Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.
- 3. Mamlaka ya mhubiri yanapatikana katika mamlaka ya Neno la Mungu.

Mhubiri ni lazima aelewe kwamba Biblia siyo maneno ya wanadamu bali ni

Neno la Mungu lenye nguvu. Neno lenye nguvu maana yake *Mungu amelivuvia*. Mungu aliwawezesha waandishi wa Biblia; ndio kusema kwamba, Mungu **alipumua** kupitia watu hao Neno la uhai. <u>Biblia Haijahusisha Neno la Mungu peke yake bali ni Neno la Mungu</u>.

II Petro1:21 – Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

#### C. Wito wa Mungu

1. Kazi ya kuhubiri ni wito wa Mungu.

Kila mwanadamu hakuitwa awe mhubiri, na kwa bahati mbaya wengi wanaojaribu kuhubiri hawajaitwa na Mungu. Muhubiri ni lazima awe **ameitwa na Mungu.** 

- Efe. 4:11 Na akawapa wengine, ufuasi; na wengine, unabii; na wengine, uinjilisti; na wengine, wachungaji na walimu;
  - 2. Ni Mungu peke yake anaweza kumfanya mhubiri.

Darasa hili halitakufanya uwe mhubiri. Darasa hili litakusaidia ujue namna ya kujifunza Biblia, kuandaa hotuba, na kuhubiri kile ulichojifunza. Vifaa hivi vyote havitakufanya uwe mhubiri. Mahubiri yenye maana siyo ya kuonyesha matukio tu na ukweli wa Neno la

Mungu bali ni kazi ya Roho Mtakatifu kupitia katika chombo kilichoandaliwa.

#### II. Kwa nini Ujifunze?

II Tim.2:15 - **Jitahidi** kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiyekuwa na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.

Mhubiri anahitaji uelewa mzuri wa Neno yeye mwanyewe, ili waweze kuwatangazia wengine ukweli. Darasa hili litamwezesha mwanafunzi kufahamu namna ya kujifunza Neno la Mungu na kuelewa maana ya Injili.

Nguvu ya hotuba ipo katika maandalizi. Mhubiri anahitaji ujumbe kutoka kwa Mungu. Maandishi ya Injili yanapaswa kuchaguliwa kwa maombi ya kina na kufikiri. Maandishi yakisha chaguliwa na mhubiri anapaswa kujifunza taarifa hizo za Injili. Lengo ni kufahamu unakoelekea kabla ya kufika katika madhabahu.

Darasa hili litakufundisha namna ya kuandaa ratiba ya hotuba ya msingi. Ratiba ya msingi ni njia rahisi ya kuweka dondoo za injili ambayo umeshajifunza. Ratiba hii ya msingi ni maandiko madogo ambayo inaonesha mipaka ya hotuba. Ratiba iliyoandaliwa vizuri itasaidia katika kuhubiri kwa hotuba.

Kila mhubiri atajenga muondoko wake wa kuhubiri na wa kuandika dondoo. Baadhi ya wahubiri watahubiri bila kuwa na dondoo chache na wengine wataandika taarifa zote kuhusu hotuba yao yote. Darasa hili litapendekeza njia rahisi ya kuandika taarifa kwa ufupi kwa ajili ya matumizi ya mhubiri. Wahubiri wengine wanaweza kutumia maandishi hayo kwa ajili ya matumizi yao binafsi na wasiyatumie kabisa wakiwa Mimbari. Mhubiri anaweza kutumia njia yoyote lakini ni lazima ajifunze Injili.

## Umuhimu wa Kuhubiri kwa Nguvu za Roho Mtakatifu

I. Mhubiri ni lazima ajazwe nguvu za Roho Mtakatifu.

Matendo.1:8 - Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.

Luka 24:49 - Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.

Wafuasi wa kwanza wa kanisa waliambiwa na Yesu wasubiri katika mji wa Yerusalemu mpaka watakapopewa nguvu na Roho Mtakatifu. Baada ya Yesu kumwaga damu Yake msalabani kununua wokovu wa Mwanadamu, alipaa mbinguni na kuiacha kazi ya kuieneza Injili mikononi mwa mwanadamu. Yesu alifahamu kwamba mwanadamu hawezi kuhubiri Injili na kuzifikia Roho za watu zilizopotea bila kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Aliwaambia wafuasi wake Roho Mtakatifu atawapatia nguvu ya kuieneza Injili kwa mataifa yote. Hakuna uhai wala nguvu katika maneno ya mhubiri bila upako wa Roho Mtakatifu.

A. Hakuna kilichombadala wa nguvu za Mungu katika maisha ya mhubiri.

II Kor.3:6 - "Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa Roho; kwa maana andiko huua bali Roho huhuisha."

Kujifunza na kuandalia bila kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu hakutakamilisha kazi ya mhubiri katika madhabahu. Neno andiko katika Injili linamaanisha andishi la sheria bila kuwa na Roho wa Mungu. Neno peke yake bila Roho Mtakatifu halitakuwa na uhai. Lengo la darasa hili ni kuonesha umuhimu wa kujifunza na kufanya maandalizi pamoja na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu.

B. Mwanadamu hana uwezo wa kwake binafsi wa kuihubiri Injili.

I Petro 4:11 – Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu, ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo, Utukufu na uweza una yeye hata mileke na milele. Amina.

1. Mungu alikusudia mahubiri ya Injili yafanyike kwa nguvu.

I Yoh.2:20-Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua nyote.

Neno mmepakwa katika aya hii inahusu kupataniswa na Mungu. Neno hilo lina maana ya kile kinachotumiwa kufanya upako. Mito ya uhai inayomwagika kutoka kwa mhubiri itawafikia wanadamu wenye kuhitaji. Neno kupakwa maana yake ni kuchafua. Kwa lugha ya asili ya Kiyunani; linaelezea kuenea kiasi cha kutosha kwa uwepo wa Mungu kunakomsaidia mwanadamu kuhubiri kwa nguvu na mamlaka.

2. Mungu huwapa uwezo wa kuhubiri wale anaowaita kuwa wahubiri wa Injili.

Uwezo asilia peke yake hautoshi kuifikia mioyo ya wanadamu. Mbinu za kuongea na kupamba maneno hazitazaa uhai. Mhubiri anapaswa kuwa na upatanisho na Mungu ndipo aweze kutangaza Neno la Mungu.

C. Mtume Paulo alipewa nguvu na Roho Mtakatifu.

I Kor: 2:4,5 - Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za

Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

Paulo alihubiri kwa nguvu za Mungu. Neno linatuambia kwamba nguvu hizo zilidhihirika wazi wazi. Kudhihirika ni kwa kitu kinachoonekana. Dunia inahitaji kuoneshwa zoezi la nguvu za Mungu. Paulo hakutegemea hekima ya mwanadamu kulihubiri neno la Mungu. Paulo alikuwa ni mtu mwenye elimu. Alikuwa ni Mfarisayo aliyefundishwa sheria ya Musa na Gamalieli ambaye alikuwa daktari wa sheria. (Mdo. 5:34; 22:3) Hata hivyo Paulo pamoja na mafunzo aliyokuwa nayo alizihitaji nguvu za Roho Mtakatifu katika kazi ya kuhubiri Injili.

- II. Upako wa Roho Mtakatifu: Maneno haya yana maana gani?
  - A. Mafuta ni alama ya Roho Mtakatifu.

Katika Maandiko Matakatifu mafuta ni alama ya Roho Mtakatifu. Mafuta anayomiminiwa mtu ni alama ya Roho Mtakatifu anayemiminwa katika maisha ya mtu huyo.

B. Neno hili linahusu nguvu za Roho Mtakatifu zinazokuja juu yake na kuenea katika nafsi yake.

Yesu alisema Roho Mtakatifu atamwagika kutoka ndani yake mwanadamu kama mito ya maji yenye uhai - Yoh. 7: 38-39. Katika Agano Jipya kupakwa mafuta kunatumika kuonesha uhusiano wake na mahubiri ya Injili. Kupakwa mafuta ni kupewa nguvu za Mungu ili kumwezesha mwanadamu afundishe kwa nguvu na mamlaka.

1. Katika Agano la kale wafalme walipewa mamlaka yao kwa kupakwa mafuta.

Wafalme walipakwa mafuta na manabii wa Mungu. Hii ilikuwa ni ishara kwamba wamepewa mamlaka na Mungu na kutengwa kwa ajili ya huduma yake. Mpango wa Mungu kwa wafalme hawa ni kuwapatia Roho Mtakatifu katika maisha yao. Baadhi ya wafalme hao hawakumtumikia Mungu kwa hiyo Roho Mtakatifu hakuwa pamoja nao.

2. Katika Agano la Kale manabii walipakwa mafuta.

I Wafalme 19:16 - Na Yehu mwana wa Nimshi mtie mafuta awe Mfalme wa Israeli; na Elisha mwana wa Shafati wa Abel-Mehola mtie mafuta awe Nabii mahali pako.

Katika Maandiko nabii Elisha anaagizwa na Mungu ampake mafuta Yehu awe Mfalme naye Elisha apakwe mafuta ili awe Nabii mahali pake. Mafuta haya yalimwagwa juu ya Manabii kama alama ya Roho Mtakatifu akiwa amemwagwa katika maisha yao. Manabii waliongea kama kipaza sauti cha Mungu. Mungu aliongea kwa midomo ya Manabii; hawakusema mawazo yao wenyewe walipotabiri ila walifanya hivyo Mungu alipozungumza kupitia kwao. Biblia inatumia maneno: "Neno la Bwana," katika kuelezea Mungu alivyofikisha ujumbe kwa kuwatumia Manabii wake - Yeremia 44:22

3. Katika Agano la kale Makuhani walipakwa mafuta.

Hesabu 3:3 - Hayo ndiyo majina ya wana wa Haruni, hao makuhani waliotiwa mafuta ambao aliwaweka wakfu ili wafanye kazi ya ukuhani.

Makuhani hawa walipaswa kuwa Watakatifu katika Bwana. Walipakwa mafuta pia. Hii inatuonesha kwamba wale ambao wanafanya kazi ya Bwana wanapaswa kumwagiwa Roho Mtakatifu.

4. Mungu alimpaka mafuta Yesu ndipo akaifundishe Injili.

Luka 4:18,19 - Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru walioteswa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.

Waebrania 1:9 - Umependa haki, umechukia maasi; kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, mafuta ya shangwe kupita wenzio.

Mwana wa Mungu alipewa nguvu na Roho Mtakatifu kuihubiri Injili. Tunahitaji kuongezewa kupakwa mafuta kiasi gani ili tukaihubiri Injili?

Mathayo 7:29 - Kwa maana alikuwa akitufundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.

Yesu aliongea kwa mamlaka. Mungu hutoa mamlaka kwa mhubiri kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

C. Kupakwa mafuta huvunja vifungo vya dhambi.

Isaya 10:27- Tena itakuwa katika siku hiyo mzigo wake utaondoka mabegani mwako, na nira yake shingoni mwako, nayo nira itaharibiwa, kwa sababu ya kutiwa mafuta.

Isaya 61:1- Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma

ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao;

Kupakwa mafuta huharibu vikwazo vya kifungo. Watu wamefungwa kwa dhambi na ni nguvu ya Mungu peke yake inayoweza kuwaweka huru. Yesu alisema kupakwa mafuta kutawaletea mateka uhuru. Watu wengi wamefungwa kwa nguvu za shetani na kuwekwa katika gereza la dhambi. Neno la Mungu likihubiriwa na mpakwa mafuta na Roho Mtakatifu litavunja minyororo ya vifungo na kuwaweka watenda dhambi huru na nguvu za shetani.

1. Nguvu za Roho Mtakatifu huwepo wanapokusanyika waumini.

Roho Mtakatifu anao uwezo wa kuvunja nguvu za dhambi wakati mhubiri anakihubiri. Kuhubiri hakuwezi peke yake kuvunja nguvu za dhambi. Upako wa Roho Mtakatifu ndio utakaovunja nguvu za dhambi katika maisha ya wanadamu. Upako ni zaidi ya nguvu za Mungu katika kumsadia mhubiri na ni nguvu za Mungu katika kulisaidia kusanyiko.

2. Roho Mtakatifu huleta ondoleo la dhambi.

Yohana 16:8 - Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu:

Roho Mtakatifu atawashawishi wanadamu wakubali dhambi zao kisha atawasogeza katika msalaba. Mahubiri ya mpakwa mafuta yataleta ondoleo la dhambi. Mwanadamu anaweza kulihubiri Neno, lakini ni Roho Mtakatifu peke yake anayeweza kuwafanya wanadamu watambue dhambi zao na kuwapeleka kwa Mungu.

## Mafundisho ya Neno la Mungu

Yeremia 3:15 - Nami nitawapa ninyi wachungaji wanipendezao moyo wangu, watakaowalisha kwa maarifa na fahamu.

Kazi ya mhubiri ni kuwalisha watu ukweli wa Neno la Mungu. Mhubiri anapaswa kuwafanya watu waweze kuielewa vema Biblia. Ni lazima mhubiri alielewe Neno yeye mwenyewe ndiyo aweze kuwahubiria watu wengine. Nehemia alisoma katika kitabu cha sheria, halafu akawaeleza watu maana yake ili waweze kuelewa Neno la Mungu kwa ajili matumizi yao wenyewe. Hii ndiyo maana ya mahubiri: kutangaza Neno la Mungu kwa njia ambayo watu watalipokea, watalielewa, watashawishika na kulifanyia kazi. Lengo la darasa hili ni kuwasaidia wanafunzi waweze kufahamu namna bora ya kujifunza Neno la Mungu. Hakuna njia maalumu iliyopangwa ya kujifunza; kila mhubiri ataweka utaratibu wake wa kujifunza Maandiko Matakatifu. Mhubiri anapaswa kujenga tabia ya kusoma Biblia kila siku. Mhubiri anapaswa kulijua Neno kabla ya kwenda kulihubiri.

I. Mhubiri anapaswa kuelewa maana ya taarifa za Biblia.

II Petro 1:20 - ...hakuna unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama apendavyo mtu fulani tu..

A. Kuna maana moja tu kwa taarifa zilizopo katika Biblia.

Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu, na Mungu anafahamu kwamba alikuwa na maana gani alipompatia mwanadamu Neno lake. Roho Mtakatifu atamwezesha mwanadamu kulielewa Neno. (Yohana 16:13) Mwanadamu hatapata uelewa mara moja wa Neno la Mungu. Mhubiri anaposali, na kujifunza Neno la Mungu, Mungu atamsaidia aweze kulielewa zaidi. Mhubiri ni sharti awe na uelewa angalao wa taarifa anayokusudia kuihubiri.

D. Siri ya kutafsiri kwa usahihi Biblia ni kuelewa vizuri taarifa kama ilivyoandikw

Taarifa kama ilivyoandikwa ni jinsi neno au sentensi ilivyowekwa kuhusiana na sentensi nzima au taarifa yote. Njia bora ya kufahamu maana ya neno ni kuona jinsi neno hilo lilivyotumiwa katika sentensi.

E. Kamusi inaweza kumsaidia mhubiri kujipatia uelewa mzuri zaidi wa Neno la Mungu.

Vipo vitabu vya rejea vinavyopatikana kama kitabu cha **Strong** kiitwacho <u>Ufanuzi Kamili wa Biblia</u> (Exhaustive Concordance) na kitabu cha **Vine** kiitwacho <u>Kamusi Bayana</u> (Expository Dictionary) vitatusaidia kuelewa kwa lugha asilia ya Kiyunani au Kigriki kama ilivyo katika Maandiko. Vitabu hivi vinazo maana za maneno katika lugha za asilia. Matumizi ya kamusi za lugha za kawaida kama <u>Webster</u> kunaweza kutusaidia kuelewa maana ya maneno yaliyopo katika Injili. Kwa mfano neno "mtumishi" katika Warumi 1:1 ni *doulos* katika lugha ya asili ya Kigiriki na maana yake ni "mtumishi kwa mapenzi yake" au "mtu aliyejichagua mwenyewe kuwa mtumishi." Paulo anasema kwamba yeye ni mtumishi wa kujichagulia mwenyewe na kwa kupenda siyo kwa kusukumwa kwa uzito wa dhambi zake. Kuangalia maana ya neno "mtumishi" kutasaidia kuelewa maana sahihi kwa maelezo yaliyopo.

#### II. Mhubiri anapaswa kulinganisha Andiko kwa Andiko.

I Wakorinto 2:13 - Nayo twayanena, si kwa maneno yaliyofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.

Mafunzo ya Biblia hutumia mbinu ya kulinganisha Andiko kwa Andiko. Biblia inatuagiza kulinganisha vitu vya rohoni kwa mambo ya rohoni. Kama ukilinganisha aya ya Biblia na aya ya Biblia utaeleweka vizuri zaidi. Neno la Mungu litaonekana vizuri kama vipande vya fumbo moja. Andiko moja litafafanua Andiko lingine. Biblia inafaa kuilinganisha yenyewe. Hakuna mgongano katika Biblia. Alichoandika Mungu katika kitabu cha Mwanzo kinaelewana na alichoandika Mungu katika kitabu chaUfunuo.

A. Linganisha maandishi ya Neno la Mungu yanayohusu somo moja.

Itifaki ni kitabu cha orodha ya maneno katika Biblia na huonesha ni wapi yalipo ndani ya Biblia. Tumia itifaki kupata Injili zinazolihusu somo moja. Kwa mfano kama somo la kufunga limechaguliwa; utatafuta Maandiko yenye neno kufunga, funga au ufungaji na usome maandiko hayo ambayo yataelezea kuhusu mafungo. Hii itampatia mhubiri uelewa wa Biblia wa somo hilo na kumwonesha chanzo cha maneno ya kutumia awapo katika mimbari.

B. Linganisha jinsi Neno moja linavyotumika kwa Maandiko tofauti tofauti.

Njia nzuri ya kuelewa maana ya Neno ni kuona jinsi Neno hilo linavyotumiwa katika taarifa tofauti za Injili. Kwa mfano, angalia jinsi

"Neno" linavyotumika katika Yohana 1:1 na 1:14 na utaelewa kwamba "Neno" ni kumhusu Yesu.

C. Andiko litajieleza lenyewe kama aya za Biblia zinavyolinganishwa.

Neno la Mungu linao umoja kulihusu Neno lenyewe. Aya za kitabu kimoja cha Biblia zitaunga mkono ukweli unaopatikana katika aya nyingine za Biblia. Aya moja inaweza kusaidia kueleza maana ya aya nyingine. Kwa mfano

I Wakorinto 12:13 - Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja.

Waefeso 1:22-23 – Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake, anayekamilika kwa vyote katika vyote.

Waefeso wanaeleza kwamba kanisa ni mwili wa Kristo; na kwa kulinganisha aya hizi na I Wakorinto 12 tunaelewa kwamba "mwili" ni kuhusu "kanisa" katika aya zote mbili.

- III. Mhubiri anapaswa kuandika kwa kifupi kitu alichojifunza.
  - A. Andika maana ya maneno mapya au yasiozoeleka.

Kila mmoja atajenga utaratibu wake mwenyewe wa kujifunza maneno mapya. Baadhi ya maneno ya Biblia yanayo maana tofauti katika lugha ya asili zaidi ya maana yake ya leo. Njia mojawapo ni kuwa na daftari ndogo ya maneno mapya na ufafanuzi wa maneno ya Biblia; hii itakusaidia kukumbuka maelezo yake. Jinsi muhubiri anavyoelewa zaidi kuhusu Neno la Mungu ndivyo Mungu anavyoweza kumtumia awpo katika mimbari.

F. Taarifa unazojiandikia katika daftari ziwe katika lugha rahisi, wazi na zenye lengo.

Sio lazima uandike kitabu ili kuwa na taarifa nzuri. Panga taarifa zako kwa mada na masomo. Weka orodha ya aya muhimu za maandiko zinazohusiana na somo lako. Iwapo utatumia maandishi katika mimbari hayapaswi kuwa na kila kitu ulichojifunza. Taarifa za somo zinapaswa kuwa fupi fupi na zenye mpangilio. Katika darasa hili tutajifunza namna ya kuandaa ratiba rahisi ya somo la kutumia katika mimbari.

C. Andika wazo au kichwa cha somo mapema utakavyoweza.

Kama hutaandika kitu mara unapokipokea unaweza usikikumbuke baadaye. Mungu anaweza akakuonyesha kitu ukiwa katika maombi au unapolisoma Neno; mambo haya yanapaswa kuandikwa na kuhifadhiwa ili uweze kujifunza au kuyatumia baadaye.

D. Unaweza kupata faida kwa kuitenganisha Injili katika mawazo yake.

Njia nzuri ya kusoma Injili ni kuitenga katika mafungu yake muhimu kama ilivyoandikwa. Unaweza kuendelea kujifunza wazo kuu la kilichoandikwa peke yake. Lengo la mhubiri ni kushirikisha wengine sehemu moja ya ukweli au tukio kwa wakati mmoja. Kuigawa Injili katika vipande kutakusaidia kuhubiri sehemu moja ya Injili halafu ukaendelea na sehemu nyingine kisha ukaijenga yote kwa wakati. Kwa mfano Yohana 3:16 inaweza kutenganishwa katika mawazo yake makuu kama ifuatavyo:

Sehemu ya Injili	Mada ya Kujifunza
Kwa jinsi hii Mungu aliupenda	<b>upendo wa ajabu</b> wa Mungu -
ulimwengu	anawapenda wote
hata akamtoa Mwanaye wa pekee	Gharama kubwa ya wokovu wetu -
	msalaba
ili kila amwaminiye	<b>mahitaji makubwa</b> - Imani
asipotee	kuepuka kabisa - kutotiwa hatiani
bali awe na uzima wa milele	Zawadi kubwa - Mbinguni

Ukiangalia sehemu ya aya hii na ukajifunza utaielewa vizuri zaidi aya yote. Hii itakusaidia pia kuihubiri kwa kipande kimoja baada ya kingine. Utajifunza maana ya kushirikisha wengine sehemu kwa sehemu na kujenga hatua moja kwa wakati mmoja.

### Kutoa Hotuba

Sehemu hii itaangalia mbinu mbalimbali za kutoa hotuba. Hatupendi sote tuingie katika mtego wa kutoa hotuba (kuongea kwa werevu wa kisomi), lakini kuna mbinu fulani ambazo mhubiri anaweza kujenga ili zimsaidie katika mahubiri ya Injili. Kuhubiri ni jambo la kuongea hadharani na Mungu huwapatia zawadi na vipaji wanadamu ambao anaweza kuwatumia kueneza Injili.

- I. Mhubiri anapaswa Kujitegemea.
  - A. Usijaribu kumuiga mhubiri mwingine.

Usijaribu kuwa mtu tofauti. Baadhi ya watu hujaribu kuiga matendo na miondoko ya wahubiri wengine au hujaribu kuiga sauti ya mhubiri mashuhuri kwa kudhania kwamba kufanya hivyo watakuwa na Roho sahihi na yenye kuvutia. Hii siyo njia sahihi ya kulihubiri Neno la Mungu. Njia sahihi ya kuhubiri ni kuuacha muonekano wako uwe kwa Roho Mtakatifu.

#### G. Unapaswa kuonekana asilia katika mimbari.

Usijaribu kulazimisha kitu kisichokuwa asilia kionekana. Usirushe mkono wako ili kuonekana ukifanya chochote. Acha mikono yako ifanye mambo yanayoonekana ya asili, ikiwa imelegea na siyo migumu au iliyolazimishwa. Mhubiri anaweza kupiga kelele na kuruka ruka kuhusu kinachohubiriwa na upako utampatia nguvu na mamlaka pia yatakuwepo katika sauti lakini tumia sauti yako binafsi kila mara uwapo katika mimbari. (Unahubiri Injili siyo kwamba unafanya maigizo.)

#### C. Mungu atautumia muonekano wako.

Muonekano wa mhubiri utakuwa dhahiri katika mimbari. Mungu atakutumia kama ulivyo kulitangaza Neno lake.

## IV. Epuka Tabia za Kuchanganyikiwa ambazo zitakupotezea ule Ujumbe.

Tutajadili mambo machache yanayofanywa na watu wengi ambayo huharibu kitu kinachosemwa ili upate kujua ni nini cha kuepuka unapohubiri. Ziko tabia nyingine zinazofanana na hiyo ambazo hata wahubiri wazoefu hujikuta zikiwasumbua:

#### A. Usiweke mikono yako mifukoni mwako.

Watu wengine hufanya kitu kabla hawajatulia kwa sababu hawajafahamu vizuri ni nini cha kufanya. Baadhi ya wahubiri huchezea sarafu mifukoni mwao au funguo wakati wakiwa wanahubiri. Tabia za namna hiyo huwa zinasumbua sana na zinaweza kukuzuia kupokea kile Mungu anachotaka ukifikishe katika mioyo ya watu.

- H. Usichezee vidole vyako. Kitu kidogo kama kuchezea vidole vyako kinaweza kukuharibia sana mahubiri.
- I. Usiseme *aah...* au *umm...* unapohama kutoka wazo moja kwenda wazo lingine.

Watu wengine wanayo tabia ya kujaza mianya kama hiyo kwa kuingiza ndani miguno isiyoeleweka wakati wanapoongea. Tabia za

namna hii zinaweza kukuchukua muda mrefu kuziondoa, lakini ni muhimu kujitahidi kuziacha kabisa unapokuwa katika mimbari. Siyo vibaya kupumzika kidogo wakati unapohubiri. Wakati mwingine mapumziko ya namna hiyo yanaweza kuwafanya watu watulie zaidi. Ni bora kupumzika kuliko kujaribu kujaza nafasi hiyo kwa maneno ambayo hayana maana na wala usiongeze chochote katika ujumbe uliokuwa nao.

#### J. Usitembee tembee kwa kasi wakati unapohubiri.

Siyo vibaya kutembea na kwenda hatua chache wakati unapohubiri na wakati mwingine mhubiri anaweza kuteremka kutoka katika jukwaa na kuchanganyika na watu huku akiwa anahubiri. Kunayo tofauti hata hivyo kati ya kutembea kama kawaida na kutembea kwa kasi. Mnyama aliyefungiwa kwenye kisanduku atakimbia huku na huko kwa lengo la kwenda mahali popote. Miondoko inayofanana na simba aliyefungiwa kwenye kisanduku wakati ukiwa unahubiri itahamisha akili za watu katika mahubiri yako.

## III. Kuwaangalia watu machoni ni jambo zuri katika utoaji wa hotuba.

#### A. Usiangalie chini unapohubiri.

Baadhi ya wahubiri huwa na ujumbe mzuri lakini watu wanapata shida kuupokea kwa sababu mhubiri anaangalia chini kila wakati anapokuwa akiongea. Ni muhimu sana kwa mhubiri kutoonekana akidodosa alichoandika kwenye kijidaftari chake wakati akihubiri. Taarifa za namna hiyo zinapaswa kutupiwa jicho kwa haraka mara moja moja wakati wa hotuba. Unaangalia andiko lako halafu unawaangalia watu na kuwahubiria. Andiko lako linapaswa kuwa fupi tu kwa ajili ya kukusaidia kukumbuka kitu ulichojifunza na kuongezea Maandiko kuupa nguvu ujumbe wa hotuba yako.

#### B. Angalia watu machoni unapohubiri.

Kuhubiri ni kuwafikishia watu ujumbe wa kweli. Mtu anayefanya mawasiliano kwa njia nzuri huangalia watu machoni anapoongea nao. Kukiwepo na mkusanyiko mkubwa haitawezekana kuangalia kila mmoja machoni, lakini bado mhubiri anahitaji kuangalia watu wakati akihubiri. Kukutana kwa macho hufanya anayesikiliza aone kwamba unaongea naye!

#### IV. Kauli sahihi ni Muhimu kwa ajili ya Ujumbe kueleweka.

#### A. Usitafune maneno wakati unapoongea.

Ni vema ukaongea vizuri na kutamka kila neno ili watu waweze kuelewa kitu unachosema. Fanya mazoezi ya kutotafuna maneno katika mazungumzo yako ya kila siku; hii itakufanya uwe na tabia ya kuongea sawasawa. Vilevile hii itawaondolea watu usumbufu wa kugeukiana na kuulizana mara kwa mara, "Amesema nini?"

B. Ongea kwa sauti kubwa na ya kutosha ili watu wasikie kitu unachosema.

Hata kama utatumia kipaza sauti na vifaa vya namna hiyo unapaswa kuongea kwa sauti ya kueleweka. Wasemaji wazuri huweka sauti yao sambamba na sehemu ya kati ya kisehemu cha kuongelea. Fanya mazoezi ya kuelekeza sauti yako na ruhusu hewa itoke ndani ya mapafu yako.

#### V. Hubiri kwa Moyo.

A. Watu wanahitaji kuamini kwamba wewe unaamini unachohubiri.

Unajaribu kuwashawishi watu kuamini kwamba Neno la Mungu ni ukweli na wao wanalihitaji katika maisha yao. Inapaswa kusiwepo na shaka au maswali katika akili ya mhubiri anapolitoa hadharani Neno la Mungu. Kusanyiko litachukulia kusita kwako kwa uzito na kutomwamini mhubiri. Kama unayo mashaka au maswali unahitaji kufanya maombi mpaka upate uthibitisho wa Mungu moyoni mwako kuhusu Neno unalotegemea kuhubiri.

K. Hubiri kwa hisia na msukumo.

Ni vizuri ukisisimka kuhusu unachohubiri. Yesu alikuja kutupatia uhai. Mhubiri anapaswa kuwa amejaa uhai wa Yesu.

#### VI. Kutupa Mikono na Kusogea

Ni sawa kutumia mikono wakati unapohubiri. Unahubiri Neno ambalo liko hai; huhitaji kukauka na kuonekana kama uliyekufa uwapo katika mimbari. Kama ulikuwa unaelezea hadithi ya Daudi na Goliati, ni vema ukiamua kuuzungusha mkono wako juu ya kichwa chako kama unayetupa jiwe. Kurusha mikono kunaweza kukusaidia unapowahubiria watoto lakini ni muhimu pia kwa mahubiri ya watu wazima.

A. Kupeleka mkono huku au kule kunaweza kukakuongezea uwezo wako wa kufikisha ujumbe.

Mzungumzaji mzuri huonesha kwa mikono yake wakati anapoongea. Lengo letu katika kuhubiri ni kumzidi mhamasishaji yeyote ijapokuwa tunataka kutumia kila njia iwezekanayo kuupeleka ukweli wa Neno la Mungu kwa watu. Iache mikono yako ifanye kile kitakachoweka uzito katika ujumbe. Hupendi kurusha rusha mikono bila kuwa na lengo au sababu. Kwa watu wengine matumizi ya vitendo vya kuonesha kwa mikono wanapoongea ni jambo la kawaida kwao wakati kwa wengine itaonekana wanajilazimisha kuchora chora kwa mikono yao. Unalazimika kukumbuka kwamba wewe utaendelea kuwa wewe, lakini siyo vibaya kujieleza kwa kupeleka peleka mikono.

L. Kufanya matendo fulani kunaweza kukasaidia kuchora wazo lako.

Unaweza kutumia matendo kuonesha unachoshirikisha watu wengine. Kwa mfano unaweza kushikilia juu ngao ya imani au ukafanya matendo kama unaye zungusha upanga kuweka picha ya upanga wa Roho akilini mwa watu. Unajaribu kuwashawishi watu kuhusu mahitaji yao na unawashirikisha ukweli huo; unaweza kutumia njia yeyote ile kuweka uzito katika wazo ulilo nalo. Usingependa matendo ya namna hiyo yazidi kiwango hadi yakuhamishe kutoka katika kinachosemwa, lakini ni vyema kutia uhai na nguvu katika somo.

### Wasifu wa Mhubiri

Kiwango cha uwezo wa mhubiri kinapimwa kwa akili, kwa maadili na kiroho. Mhubiri anapaswa kuwa amehitimu kiroho na anao upako wa kuhubiri. Mhubiri anapaswa kuwa amehitimu katika mafunzo yake ya Biblia. Mhubiri anapaswa pia kuwa msafi kimaadili na uwepo ushahidi wa Kikristo. Sasa tuangalie kwa makini wasifu bayana wa mhubiri.

#### I. Anapaswa kuwa Mkristo wa Kweli.

Ili kumhubiri Kristo ni lazima umjue Kristo. Paulo alisali na kusema: *ili niweze kumjua Yeye*. Kama mhubiri unahitaji kumjua Kristo kama Mwokozi wako. Unalazimika kumjua Kristo ni nani ndio uweze kuwaeleza wengine Yeye ni nani. Ni wazi kwamba mhubiri ni lazima awe amezaliwa mara ya pili ingawa wengi siku hizi hata wale ambao bado hawajaokolewa hujiita wahubiri.

Charles Wesley, ndugu yake Yohana Wesley, alihubiri na kufundisha kwa miaka mingi kabla hajamkubali Kristo kama Mwokozi wake. Kama mdhambi, alianza masomo ya dini katika Kanisa ka Kristo huko Oxford mwaka 1726 lakini alipoteza nguvu zake nyingi akitafuta namna ya kujifurahisha. Alipata shahada yake ya uzamivu kwa kufaulu vizuri kama msomi mwaka 1733, na mwaka 1735 aliapishwa kuwa Mchungaji katika Kanisa la Anglikana. Mwaka 1738, Charles "alipata uamsho" aliokuwa anauhitaji sana. Mwishowe baada ya miaka 12 ya mafunzo marefu ya dini na hata mahubiri pia aliukubali ujumbe wa

Agano Jipya kuhusu wokovu. Charles aliyekuwa hajapata matunda yoyote na wala hakuwa msaada katika miaka hiyo 12, baada ya kuokoka alikuwa sehemu muhimu ya uamsho mkubwa nchini Amerika na alifanya kazi pamoja na ndugu yake Yohana Wesley aliyekuwa mashuhuri sana. "Kazi yake kwa miaka iliyofuata iliweza kuandika nyimbo 6,500 kulieneza Agano Jipya kama alivyolielewa." Wakati alipofariki Machi 29, 1788 alijulikana kama mhubiri mwenye nguvu na hekima.<sup>1</sup>

Ni lazima uamini kabla ya kuwa mhubiri.

I Wakorinto 4:13 - *Tukisingiziwa twasihi; tumefanywa kama takataka za dunia, na tama za vitu vyote hata sasa;* 

#### V. Anapaswa kuwa Amejazwa Roho Mtakatifu.

Matendo 1:8 - Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.

A. Mhubiri anahitaji kujazwa Roho Mtakatifu ili kuhubiri kwa nguvu.

Mhubiri hawezi kulitoa Neno kwa nguvu na mamlaka bila msaada wa Roho wa Mungu.

M. Mhubiri ni cheche tu ya anachoweza kuwa bila upatanisho na Roho Mtakatifu.

Mhubiri asiyekuwa na upatanisho ni karibu na kitu kisichokuwa na thamani. Wako wahubiri ambao wamekaukiwa na ni sawa na wafu kwa mafanikio yao kidogo au kushindwa kabisa kwa sababu ya kutokuwa na upatanisho na Roho Mtakatifu. Mbaya zaidi kuliko "kuwa na mafanikio kidogo" ni mizigo iliyooteshwa ndani ya maisha ya watu kwa unajisi wa wahubiri hao wanaoongozwa na matakwa yao wenyewe. Mhubiri anahitaji kujazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

#### III. Anapaswa kuwa na Wito

Warumi 10:15 – Tena wahubiri je wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!

A. Ni nini maana yake wito wa Mungu?

<sup>&</sup>lt;sup>1</sup> "Charles Wesley". 2005. <a href="http://www.bookrags.com/biography/charles-wesley/">http://www.bookrags.com/biography/charles-wesley/>.

Ni ukubali wa ndani anaopewa mwanadamu na Roho Mtakatifu ambo huthibitishwa kwa Neno la Mungu na Mwili wa Kristo. Roho Mtakatifu ataongea na moyo wako. Paulo alizungumza kuhusu Roho Mtakatifu kushuhudia pamoja na dhamiri yake. – Warumi 9:1 Mungu atawasha wito wake katika moyo wako. Neno la Mungu litaimarisha kukubali kwako. Mungu ataongea na wewe kwa Neno lake. Wakristo wengine waliojazwa Roho Mtakatifu watashuhudia wito wako. Roho Mtakatifu aliongea na kanisa la mwanzo kuwatenga Paulo na Barnaba kwa ajili ya kazi ambayo Mungu alikuwa amewaita waifanye – Matendo 13: 1-3 Wito wa Mungu utathibitishwa kwa Mwili wa Kristo. Yakobo, Petro na Yohana walitambua wito wa Mungu kwa maisha ya Paulo.

- Wagalatia 2:9.

#### N. Kuihubiri Injili ni wito.

Biblia inatueleza kwamba ni sharti mwanadamu atumwe ili akaihubiri Injili. Ni Mungu ambaye hutuma. Watu wengi ambao hawajaitwa wanajaribu kuhubiri Injili. Mungu alimwita Yeremia kuwa Nabii kabla hata hajazaliwa. "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa Nabii wa Mataifa." – Yeremia 1:5 wito wa Mungu ni zaidi ya hisia na msisimko. Mungu wa mbinguni atauweka wito wake katika maisha ya mwanadamu akaihubiri Injili Yake.

#### IV. Ni lazima awe Mwanafunzi wa Biblia.

II Timotheo 2:15 - Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukutumia kwa halali neno la kweli.

A. Yeyote ambaye ameitwa kuihubiri Biblia ameitwa pia kujifunza Biblia.

Ni lazima mhubiri ajue ni kitu gani anachohubiri. Paulo alimwambia Timotheo alihubiri Neno. Ni lazima ulijue Neno kabla hujaanza kulihubiri Neno. Mtenda kazi atajifunza na kuelewa kazi ambayo anategemea kuifanya. Kwa mfano fundi magari atajifunza kuhusu magari, seremala atajufunza namna ya kufanya kazi kwa mbao, na mhubiri anapaswa kama yule mtenda kazi mwingine ajifunze Neno la Mungu ambalo anategemea kulihubiri.

#### B. Inabidi mhubiri ajenge tabia ya kujifunza Biblia kila siku.

Iwapo mhubiri analishwa Neno la Mungu kila siku atakuwa na kianzio tajiri cha Mkate wa Maisha wa kuwalisha wengine. Mhubiri anapaswa kujiandaa kwa kujifunza andiko analotegemea kuhubiri kabla ya kuingia katika mimbari. Anapaswa kuwa na uelewa mzuri wa taarifa ya Injili ambayo itahubiriwa.

#### V. Ni lazima Awe Mtu wa Maombi.

#### I Wathesalonike 5:17 - Ombeni bila kukoma.

Waefeso 6:18 - Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na mkidumu katika kuwaombea watakatifu wote;

#### A. Maombi ni ufunguo wa mafanikio ya mhubiri.

Mafanikio ya mhubiri yanapimwa kwa Roho zinazookelewa na maisha ambayo yamebadilishwa kwa nguvu za Mungu, siyo kwa faida ya fedha au umashuhuri. Mhubiri anapaswa kuishi maisha ya maombi kama anategemea upendeleo wa Mungu uzifikie roho za wanadamu. Mhubiri ambaye hatajifunza kufanya maombi hatadumu katika kazi.

#### B. Utafundisha kwa kuwa mfano.

Watu unaowapatia mahubiri watakuona wewe kama mfano wao. Iwapo wataona kwamba mhubiri wao hathamini maombi basi na wao hawatafanya maombi pia.

#### C. Nguvu za Mungu huonekana kupitia katika maombi.

Iwapo mhubiri atakuwa na nguvu za Mungu katika maisha yake ni lazima awe mtu wa maombi. Kama hakuna maombi hakutakuwepo nguvu, kama kuna kusali kidogo kutakuwepo na nguvu kidogo, na iwapo kuna kusali sana kutakuwepo na nguvu nyingi. Kila mtu wa Mungu aliyepewa nguvu na Mungu alikuwa ni mtu wa maombi. Hakuna njia fupi kwa Mungu. Iwapo unataka kuihubiri Injili kwa nguvu na mamlaka ni lazima usali na kusali.

#### VI. Ni mtu Mnyoofu wa Maisha

II Wakorinto 6:17 - Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana msiguse kitu kilicho kichafu; nami nitawakaribisha.

#### A. Mhubiri anapawa kuishi maisha yaliyotengwa.

Ni muhimu sana kwa mhubiri kuishi maisha yaliyo safi. Makuhani wa Agano la Kale waliwekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Bwana. Neno wakfu maana yake ni kutengwa au kuwekwa pembeni kwa ajili ya huduma ya Mungu. Mungu anahitaji mtu wa Mungu atenganishwe na dunia. Yesu alipakwa mafuta na Mungu juu yaw engine kwa sababu alikuwa myoofu wa Moyo na alichukia uovu. - Waebrania 1:9. Moyo wa mhubiri unalazimika kuelekea mambo ya Mungu, na siyo mambo ya dunia. Nguvu ya Mungu huja katika maisha yaliyo safi.

#### B. Mhubiri anapaswa kuweka ushuhuda mzuri.

Mh ubiri ambaye haishi kwa mfano wa Kimungu atashindwa kuwafanya wengine anaowahubiria waishi Kimungu. Neno la Mungu linatuambia kwamba sisi ni Nyaraka hai, husomwa na kujulikana kwa watu wote. – II Wakorinto 3:2. Kwa mfano kama watu watamuona mhubiri wao akikasirika mara kwa mara na kuchukia hawatamsikiliza atakapowaambia wasikasirike. Watu hawatamuheshimu mtu ambaye haishi maisha yanayompendeza Mungu.

#### VII. Anapaswa kuwa Tayari kwa Utumishi.

Mhubiri 9:10- Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima huko kuzimu uendako wewe.

Neno la Mungu linatuagiza kufanya kazi kwa uwezo wetu wote; hii ni pamoja na kuihubiri Injili. Mhubiri anapaswa kuishi kwa kuzingatia afya ili awe na nguvu kwa ajili ya huduma ya Mungu.

#### A. Mhubiri anapaswa kuwa na afya njema kwa ajili ya huduma.

Ni muhimu kama mhubiri kujutunza mwenyewe. Unalazimika kujutahidi kula vizuri na kupata usingizi wa kutosha. Biblia inatuambia kwamba kuna faida katika kufanya mazoezi ya mwili. Ni vigumu kwa mhubiri wakati anahangaika, au anashindwa kupumua vizuri na anakosa pumzi wakati akijaribu kuhubiri. Inaweza kuwa vigumu pia kwa watu kupekea ujumbe wa mhubiri ambaye hushindwa kupumua mara kwa mara. Akili yako haitakuwa makini kama hutapata usingizi wa kutosha. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Mhubiri anapaswa kujitahidi kuutunza mwili wake.

B. Mhubiri anapaswa kuwa na akili timamu katika huduma.

Hupaswi kuleta matatizo yako hadi katika mimbari. Watu watajisikia kwamba kama wewe umevunjika moyo na umelemewa.

- 1. Unapaswa kumpelekea mambo yako Yesu. (I Petro 5:7)
- 2. Yesu ndiye anayebeba mizigo yetu. (Mathayo 11:28)
- 3. Paulo alituonya tuache akili ya Kristo iwe ndani yetu. (Wafilipi 2:5)

Mhubiri anapaswa kuwa na akili kama ya Kristo. Akili ya Kristo haina kukata tamaa, kuogopa, au kulemewa. Kuwa na mapumziko mazuri na chakula kutakufanya uwe na akili timamu kwa ajili va huduma.

### Kuhubiri Kikristo

Kuhubiri ni mawasiliano kwa maneno ya ukweli wa Mungu kwa lengo la kushawishi.

Ufafanuzi huu unahusu njia tatu za kufanya mahubiri.

Mambo ya Kuhubiri "Ukweli wa Kimungu" - hutuambia nini cha kuhubiri

Njia ya Kuhubiri "Mawasiliano kwa maneno" - hutuambia namna ya kuhubiri

Malengo va Kuhubiri

"Kwa lengo la kushawishi" - hutuambia kwa nini I. Mambo ya<sub>tkulhili</sub>piri

- A. Kuhubiri ni kupeleka mbele ukweli.
  - 1. Hii hutueleza ni nini tunachopaswa kuhubiri.
  - 2. Ukweli wa Kimungu unapaswa kuwa kiini cha mada ya somo.
- B. Ukomo wa mahubiri ya Kikristo

Paulo alimuagiza Timotheo alihubiri Neno. Kwa ufafanuzi mahubiri yanapaswa kuwa na ukomo katika:

- 1. KUTANGAZA NA KUSIMAMIA NENO LA MUNGU
- 2. KUFIKISHA UJUMBE TOKA KWA MUNGU KWA MWANDAMU
- 3. KUHUBIRI KUNAWAHUSU VIUMBE WA MUNGU

Njia ya Wokovu ndio somo muhimu zaidi atakalofanya. Mwanadamu anahitaji kuwa na uhusiano na Mungu na siyo kuwa na uzito wa kidini au wa kifalsafa. Mhubiri atawaagiza waumini kuhusu wajibu wa Kikristo. Mhubiri anaitwa akaihubiri Injili ya Kristo, na siyo kufundisha fasihi au vitu ambavyo ni kinyume na masomo ya Biblia.

4. MSINGI WA SOMO LA HOYUBA NI INJILI

Wakati mhubiri anapoongea kwa msisitizo, anapaswa kulipigia **NENO LA MUNGU** kelele. Upungufu wowote katika jambo hili haukubaliki kama mahubiri ya Kikristo.

- C. Kiwango cha mafundisho ya Kikristo.
  - KUWA MAKINI Usijaribu kuhubiri sana kwa wakati mmoja.
  - KUWA SAHIHI Inabidi uliweke somo katika wazo moja kuu.
  - KUWA NA AKIBA Unapaswa kubakiza cha kufundisha wakati unaofuata.

Somo siyo lazima liwe la milele bali la Kimungu!

- D. Mamlaka ya Mahubiri ya Kikristo.
- 1. LIHUBIRI NENO! Unawakabidhi wanadamu Neno la Mungu na siyo taarifa ya kwenye gazeti. Hubiri kutokana na matokeo ya msukumo wa ushuhuda wa Kimungu wa Injili. Kuamini bila shaka yeyote msukumo wa Neno la Mungu ni muhimu kwa ajili ya kuukubali ukweli wake. Tunahubiri tunachohubiri kwa sababu ni **sahihi** na tunafahamu kwamba ni sahihi kwa sababu ni **Mungu** aliyesema hivyo. Iwapo msingi wako ni *Shajara ya mwaka* au *Ensaiklopidia*, ujumbe wako hata kama utakuwa na maelezo mazuri utakosa **mamlaka**.

Msukumo wa Neno la Mungu katika Biblia ndio unaoyapa mahubiri ya Kikristo **mamlaka** yake.

II Timotheo 4:2 - <u>Lihubiri Neno</u>, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.

2. LIJUE NENO! Ni lazima ujifunze Neno la Mungu kwa sababu unapaswa kuelewa taarifa inayoenda kuhubiriwa. Uelewa wa taarifa hiyo utampatia mhubiri mamlaka wakati wa kutoa ujumbe. Iwapo huna uhakika na unachosema au hujiamini katika uelewa wako wa ujumbe huo, uoneshaji wako wa somo utakuwa dhaifu. Kama huna uhakika kuhusu unachozungumzia watu hawatapokea ujumbe unaojaribu kuwahubiria.

II Timotheo 2:15 – Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiyekuwa na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la kweli.

3. WAPATI NENO LINALOWEZEKANA! Unapaswa kuwa mwelekevu na mwenye kutia moyo ukiwa katika mimbari. Hata kukemea kunaweza kuhubiriwa kwa njia ya kuelekeza. Kumbuka kwamba unajaribu kunyanyua maisha ya watu na siyo kuwahamisha katika jamii yao. Iwapo utawahamisha kutoka katika mazoea ni kwa lengo la kuwajenga upya. Usimalizie somo lako kwa njia ambayo siyo endelevu bali elekeza njia rahisi. Dakitari akishatambua ugonjwa, haondoki akaondoka nyumbani bali hufuatia kwa dawa.

Waebrania 4:12 – Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

- E. Kuna mambo muhimu ya kuhubiri ambayo humfanya mhubiri afaulu katika lengo lake la kushawishi.
  - 1. Zipo hotuba mbalimbali zinazofaa kutokana na muonekano wa eneo:
- a. **Kwa kifungu cha Maandiko** Kifungu cha Maandiko huonesha dhamira, kichwa na migawanyo. Migawanyo hupendekezwa kwa maneno muhimu katika maandishi.
  - b. **Ki mada** Msingi wake ni dhamira au somo la habari.
- c. **Kwa kifungu cha Maandiko Ki mada** Somo hutibiwa kwa kifungu cha Maandiko na kuelezwa dhamira.

- d. **Kwa kifungu cha Maandiko Kwa kilichotolewa wazo -**Somo linatokana na kilichomo ndani ya taarifa iliyoandikwa.
- e. **Kwa kufuna undani** Somo *huonesha* au *kueleza* maandishi katika utajiri wake kwa maana
  - 2. Yapo masomo tofauti ambayo yanaweza kutumiwa katika mahubiri:
- a. **Kwa Mafundisho ya Bibliia** Maagizo ya mahubiri ya mafundisho ya Biblia. (II Tim. 4:2)
  - b. **Kwa historia -** kuonesha eneo la kihistoria kuhusu taarifa ya Injili.

(kuelezea hiyo hadithi). Kuhusisha historia ili kuinua imani . (uamsho mkubwa.)

- c. **Taarifa Binafsi -** Mahubiri ya mababa wa Imani na watu mashuhuri wa Mungu.
- d. **Ufafanuzi wa Maandiko** Ufafanuzi ni maelezo au uchunguzi wa kina wa maandishi.
- e. **Kinabii -** Onyesha jinsi utabiri wa manabii ulivyotimia. Kwa kutumia maandiko onesha mpango wa Mungu kwa siku zijazo.
- 3. Somo linapaswa kuandaliwa kwa kuzingaitia umbile, maelezo kwa mpango wa wazo. Ni lazima ufahamu unakoelekea na uongoze kwa njia ambayo wasikilizaji wako wataweza kufuata!
- a. **Andishi** Chukua somo kutoka katika andishi. Usiongee tu kuhusu Biblia, *lihubiri Neno*!
- b. **Kichwa cha somo** Jina la somo huitwa kichwa. Mara nyingi kichwa ni muhimu sana katika kuonyesha mada yako kwa wasikilizaji. Siyo kila somo linapaswa kuwa na kichwa chenye kuvutia kama "Kuikimbilia ile Dhahabu," lakini somo lako linahitaji kuonesha mwelekeo karibu na mwanzoni. Kichwa ni njia rahisi ya kuwaambia wasikilizaji "huu ndio upande tunakoelekea leo."
- c. **Dhamira** Dhamira ndio somo kuu la hotuba. Somo linapaswa lisitawanyishwe, mawazo yasiyohusiana yanayoelekea kila upande, lakini kila wazo linapaswa kuunganishwa kwa dhamira moja au somo. Kuhubiri siyo maigizo ya kuchekesha ukiwa umesimama au ni wakati wa hadithi, bali ni kazi ya milele ambayo mhubiri humsubiri Mungu amletee ujumbe kwa muda huo halafu akaufuatilia kwa kina kwa uwezo wake wote wa kuwasilisha mada hiyo moja katika mahubiri yake.
- d. **Utangulizi -** <u>Waongoze</u> waumini katika somo. Usitafune maneno lakini tumia mwanzo wake kuweka msingi wa mafundisho. Egemea kikamilifu kuongozwa na Roho Mtakatifu ili aiandae mioyo na akili za wasikilizaji kupokea ujumbe wa saa hiyo.

- e. **Mwili** Ratiba ya mwili wa mafundisho inajumlisha nyama na uzito wa somo kwa maelezo ya *dondoo muhimu* au *mgawanyo*. Somo linajengeka hatua kwa hatua katika mwili wa ratiba.
- f. **Mwisho** Mwisho ni umaliziaji wa somo, lakini hujisemei tu umekamilisha, lakini huenda ni sehemu muhimu zaidi ya hotuba. Ni muhimu pia kwa sababu ni wakati mzito wa wasikilizaji kufanya uamuzi. Swali muhimu ni "Ni kitu gani kisemwe katika kumalizia?" linajibiwa kwa kujibu swali lingine, "Iwapo waumini wangeondoka wakiwa wamesahau kila kitu ambacho nimekisema katika hotuba yangu isipokuwa kitu kimoja mimi ningependa kitu hicho kiwe ni kipi?" Jibu la swali hilo **linapaswa** kuwa mada yako.

#### II. Njia ya Kuhubiri

A. Njia ya kuhubiri ni "kuwasiliana kwa kuongea." Njia ya kuhubiri inatuambia namna ya kuhubiri. Mawasiliano yanahusu kuwaeleza watu wazo. Ni lazima wazo hilo lieleweke kwa watu ndio mawasiliano yaweze kufanyika. Mahitaji ya lazima kwa mawasiliano ni maneno sahihi na kauli zilizo wazi. Mhubiri anapaswa kuongea kwa njia ambayo watu **wataelewa**. Tuangalie mfano wa Nehemia:

Nehemia 8:8 - Nao wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu kwa sauti ya kusikilika; wakaeleza maana yake, hata wakayafahamu yaliyosomwa.

Neno la Mungu lilisomwa kwa usahihi au uwazi, likaelezwa kwa wale watu au *wakawapa busara* na watu hao wakafundishwa Neno na **wakalielewa**.

Martin Luther alisema, "Ni vizuri mhubiri akihubiri na, akimaliza hotuba waumini watatawanyika wakisema, 'mhubiri alisema hivi.......'

Kazi nzuri na yenye nguvu ya mahubiri inahitaji:

- Upako wa Roho Mtakatifu, (I Yoh. 2:20)
- Lugha iwe wazi na ya kawaida (Wahubiri wenye uwezo mkubwa kama D.L. Moody waliongea katika lugha ya mtu wa kawaida.)
- ya kusisimua. (sema unachomaanisha, na maanisha unachosema.)

Ushawishi unawezekana kutokana na uwezo mkubwa. Mwishowe uwezo wa mhubiri ni matokeo ya uweza wa Roho Mtakatifu. Uweza wa Roho Mtakatifu utamfanya mhubiri afundishe

kwa hisia. Hubiri kama unayekwenda kinyume na majeshi yote ya motoni kama Daudi alivyopiga kelele katika ule mwamba, "hakuna kiini cha tatizo!" mhubiri anapaswa kuridhika na usahihi na nguvu za ujumbe wake ili kupata mafanikio. Fuata uongozi wa Roho Mtakatifu kwa sababu atakuelekeza vema na kutii uweza wake kwa sababu katika kukubali nguvu za Mungu zitaonekana wazi.

- B. Waumini wanapaswa kushirikishwa katika mchakato mzima wa hotuba.
  - Akilini mwako waweke waumini wakati ukiandaa hotuba.

Wafikirie na kuwaombea watu unaotegemea kuwapatia mahubiri. Mahubiri yenye manufaa yanamtaka mhubiri awe ni mtu anayejali na asiyekuwa mgumu wa moyo. Kuwakaribia baadhi ya watu kwa njia za uhakika huweza "kuwaweka kando". Mruhusu Roho Mtakatifu akuongoze katika maandalizi yako ya somo ili watu ambao watasikia wahisi nguvu za Mungu na kulipa nafasi somo lako. Mungu anafahamu ni akina nani watakaohudhuria na akili zao zitakuwaje na wewe pia unaweza kuona na kujifunza kitu kutokana na hali iliyopo mahali unapotoa mahubiri. Hata kama utakuwa unaongea katika ibada ya vijana wadogo, darasa la shule ya Jumapili, katika ibada ya watu wazima, katika kona ya barabara au katika hema lenye kikao cha wanauamsho; utulivu na hali ya hewa kwa ujumla ni lazima uvitilie maanani. Kwa kifupi, mhubiri ni mwanafunzi wa ubinadamu. "Mheshimiwa, siyo mambo ya kuhusu vitabu, ni wanadamu ndio tunaopaswa kuwaelewa" -Patrick Henry

2. Uweke waumini akilini mwako wakati **unapoonesha**.

Utajifunza kufahamu kama wanalipokea Neno. Unaweza kuongeza mifano mingi zaidi na kuweka uzito kama watu wanaonekana kutoolewa ujumbe. Heshimu muda uliopewa.

- C. Hotuba inapaswa kuwa ya kawaida, inayoweza kurudiwa na yenye maelezo makini.
- 1. Njia ya kawaida hutumia Maandiko kama msingi wake kwa Neno la Mungu ni sahihi na halijatenganishwa na mahitaji ya wanadamu.

Itaonekana ni jambo la kigeni (kwa usahihi kabisa) kwa waumini wa Kikristo kama Mchungaji wao atasimama na kutoa taarifa yake katika Kitabu cha <u>Uchambuzi wa Msomaji (Reader's Digest)</u>. Pili, somo linapaswa kuwa linalozoeleka. Maneno yake na maana zake ziwe rahisi kueleweka. Michoro ya matukio ya kila siku inaweza kusaidia kuwafanya watu waioanishe na somo. Yesu aliweza kutumia vizuri kile ambacho kilikuwa kimezoeleka (Kondoo, kilimo n.k.) kwa mifano wa kile ambacho hawajakizoea (Ufalme wa Mbinguni). Mifano rahisi ya

Maandiko haitawafanya washindwe kuelewa lakini, uhakikishe kwamba ni ukweli na unahusika.

2. Njia ya marudio ni tangazo rasmi la Neno.

Mpango na ratiba nzuri itahakikisha kwamba wasikilizaji wako wataweza kufuata unachohubiri. Umoja na utulivu unapaswa kujibiwa kwa mahubiri mazuri yenye hisia ya Neno la Mungu. Umbile pekee yake halitoshi lakini ni mwanzo mzuri. Kurudia kinachofahamika ni mbinu inayomsaidia mhubiri lakini kuonyesha hisia na upako kutaamua uwezo wako wa kushawishi.

3. Matumizi ya matukio yanayoeleweka huonesha vizuri ukweli wa Neno la Mungu.

Linganisha Injili na Injili nyingine na tasfiri kila taarifa kwa kutumia maandishi yake. Neno la Mungu ni Mamlaka ya Mwisho na kiwango cha kanuni za maisha. Wasiliana kwa busara na kwa njia iliyo wazi.... wewe unahitaji kuonekana una akili nzuri kwa sababu watu wanahitaji kuwa na uwezo wa kukufuata wakati unapohubiri. Waoneshe ukweli kwa njia rahisi na inayoelezeka. Washirikishe wasikilizaji wako ukweli hatua kwa hatua na jenga ujumbe huo kwa mpangilio kama somo linavyoendelea.

#### III. Malengo ya Kuhubiri

Ujumbe unatueleza **sababu** za kuhubiri. Somo limepangwa kwa mtazamo wa **kushawishi**. Malengo ambayo muhubiri anaweka mbele yake ni kama ifuatavyo

- A. **Wokovu wa Roho za Watu -** Mungu alichagua upuzi wa kuhubiri kuokoa waliopotea. (I Kor. 1:21)
- B. **Kukua Kiroho** Mungu alimelipa Kanisa Wachungaji kwa lengo mahsusi la <u>kukamilisha</u> upatikanaji wa watakatifu. (Efe. 4:11-14). Ni wajibu wa mchungaji kuwalisha kondoo kwa Neno la Mungu. (Yoh. 21:15-17)
- C. **Kuzaliwa Imani** Kwa kuhubiri Neno la Mungu, mbegu za imani zinaweza kuoteshwa katika mioyo ya watu kwa kuponya na mahitaji mengine. (War. 10:17) Mungu huhitaji imani (Ebr. 11:6) kuonekana kwa kila mmoja na wajibu wa mhubiri ni kuwafanya watu waliamini Neno la Mungu.

- D. **Liagize Kanisa** (II Tim. 4:2←Jifunze kwa moyo) lihubiri Neno uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho
- E. **Wape Moyo Waumini** Mchungaji mwaminifu wa Injili hubeba mzigo ili kila aliyeusikia ujumbe wake apate moyo na msaada. Wakati wa mahubiri, mhubiri anawafikia watu hadi wa chini kabisa kwa nguvu za Roho Mtakatifu ambapo kwa njia yoyote ile mtu atapata msaada wa kumnyanyua na kumuondoa katika shimo la kutisha.
- F. Wafanye Waumini wafikie Uamuzi Usiridhike kama muhubiri kwa kuwapa watu moyo peke yake. Iwapo wasikilizaji hawatafikishwa katika hatua ya kufanya uamuzi, wataondoka kwa njia ile ile waliyokuja nayo. Siyo wajibu wa muhubiri na hawezi kuwalazimisha watu kuwa watii, lakini anaweza kuwaongoza moja kwa moja katika mahubiri yake hadi kwenye kisima na kuwatangazia kwa ushupavu kwa mamlaka ya Roho Mtakatifu, "Kunywa! Hiki ndicho kitu unachohitaji! Njoo kwa Kristo!" Muhubiri anapaswa kufanya kazi kwa kulenga 'wito wa altareni' anapohubiri kwa sababu hapo ndipo kila mtu atapelekwa na kufikishwa katika hatua ya kuamua na ndipo wanalazimika kukubali au kuukataa ujumbe.

## Dhamira na Hoja

Utangulizi: Umuhimu wa wazo moja.

#### **KUTUNGA WAZO**

Neno *wazo* limetokana na neno la Kigiriki *EIDO*, ambalo maana yake ni *kuona na kwa hiyo kufahamu* neno linalooana na *wazo* ni *msimamo*, ambalo linatokana na tendo la kuumba. Ufafanuzi mmojawapo wa neno kuumba ni *kutengeneza picha katika akili*. Mawazo na mafikira ni lazima yaweze kuelezwa kwa maneno. Kuhubiri kunahusu mawasiliano yanayohusu msimamo wa Biblia. Njia hiyo ya mawasiliano ni wazi kwamba ni neno linalotamkwa.

## MAWASILIANO MAZURI YANAHITAJI KUWEPO NA MADA MOJA.

Mada inahusu somo kuu katika ujumbe. Ni fikra au wazo kuu ambalo linapaswa kuwasilishwa kwa watu. Utajifunza katika darasa hili kwamba matumizi ya mojawapo ya mada kuu kwa mpangilio wa Biblia ni kwa manabii na makuhani. Manabii walikuwa na ujumbe

kutoka kwa Mungu; waliutangaza ujumbe wa Mungu kwa mamlaka na usahihi. Mafundisho yaliyopo katika Agano Jipya yanayo mada moja. Muhubiri anapaswa kuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu. Ipo tofauti kati ya muhubiri ambaye anajiinulia tu andiko la kwenda kufundisha na muhubiri ambaye ana ujumbe kutoka kwa Mungu. Mungu ni Mungu wa mipango na ratiba. Mungu anao ujumbe kwa ajili ya watu; unapaswa kuujua ujumbe wa Mungu kwa wakati ambao unafanya mahubiri.

## NI LAZIMA UWEZE KUWASILISHA UJUMBE WAKO KWA WATU.

Ujumbe utakuwa na wazo moja kuu au mada; ile ambayo Mungu anataka kuwashushia watu wake siku hiyo. Hili siyo suala la kujaribu kuonesha ulivyo msomi au msemaji mzuri. Ni suala la kupokea ujumbe kutoka kwa Mungu halafu ukawahubiria watu ujumbe huo. Lengo la darasa hili ni kumsaidia muhubiri atoe ujumbe wa Mungu kwa watu. Ujumbe huo unatolewa kwa maneno.

#### I. Ni nini maana ya neno *Dhamira*?

#### A. Ni somo ambalo mhubiri amepanga kuzungumzia.

Somo hili litajibu swali: "MIMI NINAZUNGUMZIA NINI?" Mada au somo ndio mafundisho ambayo tutajishughulisha nayo. Mungu anao ujumbe gani kwa watu wake? Ujumbe huu au somo ndio kitu kinachoitwa mada.

Somo la mafundisho halipaswi kuwa neno moja tu. Neno moja haliko wazi kwa hiyo halifai kukamilisha kichwa cha somo. Neno moja kama kuabudu, imani na upendo ni mapana mno kwa ajili ya kichwa cha somo. Somo linapaswa kuwekwa wazi kwa maelezo ili kukamilisha wazo. Kwa mfano kuna pande nyingi sana za upendo ambazo zinaweza kuhubiriwa katika somo moja.

Dhamira inapaswa kutokana na taarifa ya Maandiko ambayo mhubiri ameyachagua kwa ajili ya maandishi yake. kama kawaida maandishi hayo yanapendekeza mada. Maandishi ni eneo la Maandiko ambayo husomwa kabla somo halijafundishwa. Kumbuka kwamba unafundisha Neno la Mungu. Mada inapaswa kwa asili ipatikane kutoka katika Injili. Maandishi hayo hayahitaji kutupwa kwenye ubao na kupata shida kabla ya mada kutolewa ndani yake. Mada inapaswa ionekane kwa urahisi katika maandishi kama moja ya mawazo yanayotawala. Wakati wa kulitoa somo ni vizuri kutumia mara kwa mara maneno yaliyoko katika maandishi. Kumbuka *kulihubiri Neno* kwa sababu mamlaka yako yanatokana na hilo Neno. "Ni upuuzi kufurahia maneno na kuwa mchoyo katika ukweli." - Spurgeon.

ANGALIZO: Kamusi ya Webster toleo la 10 inafafanua Neno mchoyo kama kutumia fedha kidogo sana bila kupenda.

B. Dhamira inaelezea makusudio mhubiri aliyonayo akilini mwake.

Mhubiri anapaswa kuwa na shabaha na malengo mahususi. Usifanye kazi hovyo hovyo bila kueleweka ukitegemea kupata mafanikio. Kuhubiri hufanyika kwa makini kama mlenga shabaha. Usipolenga chochote hutapiga chochote.

Lengo mahususi litakufanya utumie mada moja tu katika somo. Inawezekana kukawa na mada zaidi ya moja katika andishi, lakini haitakiwi kuwe na mada zaidi ya moja katika somo.

#### VI. Faida za kuwa na Dhamira

A. Dhamira hukuwezesha kuwa na mpangilio katika somo.

Somo halipaswi kuwa mkusanyo wa mawazo yenye uhusiano kidogo au yasiyokuwa na uhusiano wowote. Darasa hili litakupatia mafunzo ya namna ya kugawanya somo katika visehemu vinavyofaa kufanyia kazi na ambavyo vitahubiriwa kisehemu kimoja kwa wakati mmoja. Visehemu hivi vitatajwa katika darasa hili kama vipengele vya somo. Vipengele hivi vinaweza kulinganishwa na maandalizi ya chakula ambacho kinaletwa mezani kwa awamu.

Vipengele vya somo vinapaswa kuhusiana na mada kuu na kuendelezwa kama hatua zinavyofanyika katika safari. Unajenga katika ile mada hatua moja kwa wakati mmoja. Utaendelea kuifanunua mada kipengele kimoja kimoja ukihusisha na kilichotangulia kwa kuonesha uhusiano wake na mada kuu.

Mada kuu inapaswa kuwekwa akilini wakati wa kuandaa somo.

B. Dhamira kuu Huweka Umoja katika Somo.

Liache somo liwe ndio ujumbe mmoja wa Mungu kwa watu wake. Unahuhiri somo moja na siyo visomo vidogo.

Ioneshe wazi mada ya somo mwanzo hadi mwisho. Mtu aliyechelewa atakuwa na uwezo wa kutambua mada ya somo? Inawezekana wasikilizaji wako wakajibu swali hili: Mhubiri anazungumzia nini? Mada inapaswa kubaki ya mwisho na yenye picha inayotawala katika akili ya msikilizaji.

C. Dhamira husaidia kuweka wazi mtiririko wa mawazo katika somo.

Mhubiri anapawa kufafanua vizuri mada yake kama anataka somo lake lieleweke sawasawa. Usiweke mambo mengi zaidi ya yale

yanayowezekana kujadiliwa kwa wakati uliopangwa. "Anakimbiza zile nyota kumbe amekwama katika matope." - John Wesley.

Eleza kwa kifupi somo utakalohubiri. Hoja ya msingi ni maneno yanayotumika katika sentensi ambayo hueleza kwa ufafanuzi somo litakalo hubiriwa. Jambo hili litaangaliwa zaidi baadaye. Iweke mada katika msimamo unaowezekana fanyia kazi sehemu moja ya ukweli kwa wakati mmoja na hifadhi sehemu yake kwa ajili ya kipindi kijacho.

#### VII. Tukio la Biblia linalohusiana na Dhamira.

A. Manabii katika agano la kale walikuwa na ujumbe wa wazi kutoka kwa Mungu.

Ujumbe wao ulikuwa na mada moja iliyokuwa kamili kwa wakati mmoja. Kulikuwepo na lengo maalumu kwa kila ujumbe waliotoa. Lengo mahususi lilikuwa ni kushauri watu wamrudie Mungu kupitia maonyo kuhusu hukumu inayokuja na utabiri mwingine wa matukio wa siku zijazo.

B. Yesu alihubiri kwa utaratibu wenye mpangilio mzuri na Yeye ni mfano bora kabisa wa mhubiri.

Dhamira kuu inaonekana wazi katika mafundisho ya Yesu.

C. Hotuba za mitume wa agano jipya ni matangazo ya wazo moja.

Mfano uliowekwa na wafuasi wa Agano Jipya unaonesha umuhimu wa mada moja kuu. Yale mafundisho yaliilenga jamii moja na yalikuwa na ujumbe mmoja.

D. Kila kitabu cha Biblia kinaelezea mada iliyoungana.

Kwa mfano, **Zaburi** haikupangwa vibaya na mawazo yaliyopo hayakutupwa tupwa, lakini kwa kurudia rudia njia muhimu za kufanya ibada zimeelezwa.

# IV. Vipengele vya Dhamira

A. Dhamira inapaswa kuonesha kwa urahisi somo litakalohubiriwa.

Dhamari haipaswi kuwa pana mno kwa somo linalotegemewa kufanyiwa kazi katika hotuba moja. Katika hotuba moja wazo moja lililo kamilika linapaswa kuangaliwa.

B. Dhamira ielezwe kwa njia inayoonyesha wazo waziwazi.

Tumia lugha rahisi ya kawaida unapofanya mahubiri. Mada inapaswa kueleweka vyema kwa waumini.

C. Matumizi ya dhamira moja huwasaidia waumini kuelewa ukweli wa Neno la Mungu.

Dhamira moja kuu ni rahisi kukumbuka kuliko mawazo mengi yasiyohusiana. Ukijenga tabia ya kusimamia wazo moja, wasikilizaji wako watachukulia kwa usahihi uhusiano wa wazo lililooneshwa na kupata ufahamu mzuri wa ujumbe kwa ukamilifu. Iwapo wasikilizaji wako watadhani umetoka nje ya msitari au umepoteza mada yako wataacha kukusikiliza na watasubiri kwa kukosa utulivu hadi utakaporudi katika msitari wa somo lako. Watakosa mwelekeo na hamu ya kuendelea kukusikiliza iwapo watafikiri umepotea.

# V. Maelezo ya Hoja.

A. Maelezo ya hoja ni kitu gani? Maneno *maelezo ya hoja* hutumika kuelezea sentensi moja kamili ambayo hufafanua somo linaloenda kufundishwa.

Ni njia ya kueleza kwamba somo litahusu nini. Ni hotuba yote ikiwa imeelezwa katika sentennsi moja iliyo kamili. Ni njia ya kuwafanya watu wafahamu unakoelekea ili waweze kukufuata. Ni mada ambayo imeelezwa waziwazi, kwa ukamilifu na kwa sentensi inayotoa mwelekeo wa somo. *Maelezo ya hoja* yatafupisha masomo mapana.

# B. Maelezo ya hoja hukamilisha somo.

Somo haliwezi kusimama peke yake. Somo linahitaji kusaidiwa ili liwe kamili. Sentensi kamili inahitaji kuwa na mwanzo na mwisho wake. Maelezo haya yaaongezea mwisho katika mwanzo. Unatakiwa ufahamu unachoenda kusema kuhusu somo lako.

- Somo hujibu lile swali: nitaenda kusema nini?
- Maelezo ya hoja hujibu lile swali: nitaenda kusema nini kuhusu ninachoenda kusema?

Kwa mfano, maelezo ya hoja yanaweza kuwa na uhusiano na hotuba iliyopo katika kitabu cha Warumi 10:17 inaweza kuwa: Imani ya kweli huhitaji Neno kutoka kwa Mungu na utii wa kulifanyia kazi Neno hilo. Hii hujibu swali: nitaenda kusema nini kuhusu Imani? Sentensi kamili (maelezo ya hoja) hutoa mwelekeo kwa somo.

C. Maelezo ya hoja yana thamani kubwa.

Maelezo hayo ya hoja hukuwezesha kufahamu somo kamili litahusu nini? Weka ujumbe uliopokea kwa Mungu katika sentensi moja. Itakuwekea msingi mzuri kwa somo lote na kukusaidia kuweka utangulizi. Kwa sentensi moja utaweza kueleza watu unachotaka kuwafundisha. Watu watafahamu unakoenda kwa hiyo watakufuata kwa urahisi. Hali hii huwasaidia watu kuweka kumbumbu muhimu za somo na kuweza kujibu swali: "Mahubiri yalihusu nini?" Kwa kuwa watu wanaweza kukumbuka sehemu ya kitu walichosikia maelezo ya hoja huufunga ujumbe katika kifurushi cha kumbukumbu ili waweze kuchukua ukweli huo na kwenda nao nyumbani.

D. Mifano ya maelezo ya hoja iliyochukuliwa katika Maandiko ya Injili

Andiko: Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo.

- Wafilipi. 2:5

Hoja: Anayeamini anapaswa kuruhusu mawazo yake kuwa katika msitari mmoja na akili ya Kristo.

Andiko: Yesu alilia. - Yohana 11:35

Hoja: Kutoamini kwa mwanadamu kunautia moyo wa Mungu huzuni.

Andiko: Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza

ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; - Ebr. 2:Hoja: Kwa kweli wale ambao hawafanyi chochote kuhusu roho zao wanakataa zawadi kubwa kupita zote na hawataepuka hukumu ya milele motoni.

# Kifungu cha Maandiko

- I. Matumizi ya Kifungu cha Maandiko
  - A. Maana ya Neno kifungu cha Maandiko
- 1. Neno kifungu cha Maandishi mara kwa mara hutumika kumaanisha andiko ambalo husomwa na mhubiri mwanzoni mwa somo.

Ni eneo la Maandiko Matakatifu ambalo litafafanuliwa.

2. Kifungu cha maandishi kinaweza kuwa ni zaidi ya kilichosomwa.

Hotuba inaweza kujengwa kwa kuzingatia ukurasa au sura nzima. Mhubiri anaweza kuchagua kusoma sehemu sehemu za ujumbe mrefu au akapitia kwa kusoma jinsi anavyoendelea kuikamilisha hotuba yake.

3. Kifungu cha maandishi ni msingi wa Injili ambao juu yake mahubiri hujengwa.

Neno la Mungu ni mamlaka aliyonayo mhubiri - I Tim. 4:2 Neno la Mungu ndiyo mamlaka ya mwisho.

- II Timotheo 3:16 Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, linafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kuwaongoza, na kuwadabisha katika haki:
- 4. Neno la Kilatini *textus (kifungu cha maandishi)* maana yake tunda la kusuka au mtandao.

Maandishi ni nguo ya mahubiri. Mahubiri yamesukwa kuyazunguka Kifungu cha maandishi.

- B. Sababu za Matumizi ya Kifungu cha Maandiko
  - 1. Ipo mifano ndani ya Biblia ya namna ya kusoma andiko kabla ya kufundisha.
    - a. Kitabu cha sheria kilisomwa kabla ya kuwaonesha watu. (Neh. 8:8)
    - b. Yesu alisoma kitabu cha Isaya kabla ya kuwafundisha watu (Lk. 4:16-20)
    - c. Wafuasi wa Yesu walitumia maandiko kama msingi wa mafundisho yao.

- 1) Petro alimnukuu nabii Yoeli siku ya Pentekoste. (Mdo. 2:16-21)
- 2) Paulo alitumia Maandiko katika mafundisho yake. (Mdo. 13:16-42)
- 3) Timotheo alihimizwa kulihubiri Neno. 2 Tim. 4:2
- 2. Yapo matukio ya kihistoria yanayotumika ya kusoma andiko kabla ya kuhubiri.
- a. Utaratibu katika Sinagogi ulihusisha usomaji wa sehemu ya Maandiko na kufuatwa na maelezo na mahubiri ya Maandiko.
- b. Wahubiri wa kanisa la mwanzo walisoma vifungu vya Maandiko ya Injili kabla hawajahubiri.
- c. Wahubiri mashuhuri katika mikutano mikubwa ya uamsho husisitiza vifungu vya maandiko yaliyosomwa kabla ya kutoa mafundisho.
  - 3. Mamlaka ya mhubiri msingi wake ni NENO LA MUNGU.
    - a. Injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu. Rum. 1:16
    - b. Neno la Mungu halitarudi bure. Isaya. 55:11
    - c. Falsafa ya mwanadamu haitaziokoa Roho za watu.
  - C. Uchaguzi wa kifungu cha Maandiko
    - 1. Kifungu cha maandishi kinapaswa kuchaguliwa kwa kufikiria kwa uangalifu.

Fanya maombi ili upate muongozo wa Roho Mtakatifu katika kuchagua maandiko. Fikiria pia kuhusu kufaa kwa maandishi unayochagua kwa kutambua waumini utakao wafundisha. Kwa mfano wimbo wa Sulemani 1:13 hautafaa katika hotuba kwa watoto wadogo.

2. Unapaswa kuelewa mahitaji ya waumini wakati unapochagua taarifa ya Maandiko.

Kumeshatokea mikasa yoyote hivi karibuni ambayo itafanya masomo fulani yawasikitishe wasikilizaji? Kumbuka kwamba unajaribu kuwasaidia na siyo kuumiza. Wakati mwingine unalazimika kumuumiza mtu kidogo ili umsaidie, lakini haina maana kwamba kumuumiza mtu ni kusaidia. Uharibifu mkubwa umeshafanywa na wahubiri wanaotukana watu kwa Neno la Mungu.

3. Tumia kalenda ya Kikristo unapochagua kifungu cha Maandiko.

Kwenye ufufuo jumapili watu wanatarajia kusikia hotuba kuhusu ufufuo wa Kristo. Kwenye Krisimasi, siku imewekwa kusheherekea kuzaliwa kwa Kristo, unaweza kuchagua kifungu cha Maandiko kinachohusu kuzaliwa kwa Kristo.

4. Matukio ya hivi karibuni yanaweza kutumiwa kwa faida kubwa katika uchaguzi wa kifungu cha maandiko.

Maafa ya kitaifa yanaweza kuwafanya watu watambue nguvu za Mungu. Unaweza kuonesha jinsi unabii wa Biblia unavyokamilika.

- D. Faida za kutumia kifungu cha Maandiko
- 1. Kifungu cha Maandiko huonesha kwamba unazingatia ukweli na huhamasisha mshikamano na Biblia. Kifungu cha maandiko humpa mhubiri nafasi ya kuieleza Mandiko. Kifungu cha Maandiko huzuia matumizi ya maneno yaliyo kinyume na mada isiyo ya ki-maandiko.
- 2. Kifungu cha Maandiko huzuia kuropaka Kifungu cha Mandiko yataushikia ujumbe mstarinia Kifungu cha Mandiko kitamzuia mhubiri asiyumbe na kupotea njia. Njia nzuri ya kukumbuka wakati unapopoteza hatua katika mahubiri au maandalizi na kurudi katika kifungu cha Maandiko.

# VIII. Umbile la Kifungu cha Maandiko

- A. Kifungu cha Maandiko kinapaswa kukamilisha sentensi.
- 1. Iwapo siyo sentensi kamili, kifungu cha Mandiko kinapaswa kuwa na ukweli wote ambao unazungumziwa. Kifungu cha Mandiko sahihi siyo sehemu ya tamko lililotolewa katika maelezo. Sehemu za kifungu cha Maandishi zinaweza kutumiwa kwa ajili ya kitu chochote. Tafsiri sahihi ya taarifa za Biblia ni muhimu kuliko kutumia sehemu ya aya moja kama andiko.

Kwa mfano, sehemu ya Mathayo 18:17 ikitumiwa kama taarifa: "Akidharau kulisikiliza kanisa, muache yeye...". Kipande hiki cha maandishi kinaweza kutumiwa vibaya.

Weka akilini mwako ukweli mmoja ambao utauzungumzia. Mtiririko ambao andiko hilo litatokea ni lazima ufikiriwe vizuri. Hii itakulinda usifanye makosa na kuhakikisha tafsiri ya Injili inafanyika ipasavyo.

- 2. Mifano ya matumizi mazuri ya sehemu za vifungu vya Maandiko:
  - a. ...damu ya agano la milele... (Waebrania 13:20)
  - b. ...mimi ni wa nani... (Matendo 27:23)
  - c. ...tulipatanishwa na Mungu..." (Warumi 5:10)
  - d. ...utajiri usiopimika... (Waefeso 3:8)
  - e. ...wana wako, Ee Sayuni wapigane na wana wako, Ee Uyunani... (Zakaria 9:13)
  - f. ...Kila mtu kwanza huandaa divai iliyonjema;.....ndipo huleta iliyodhaifu... (Yohana 2:10)
- B. Urefu wa taarifa huamuliwa na dhamira yake.
- 1. Uwe mwangalifu kuhakikisha kwamba mada imetokana na urefu wa taarifa. Isiwe fupi mno kwa sababu haitaweza kueleza vizuri dhamira.
- 2. Taarifa fupi huvuta utulivu. Ni rahisi zaidi kwa waumini kukumbuka. Uwe mwangalifu katika kutumia taarifa fupi mno ambazo zinashindwa kukamilisha wazo.
- 3. Taarifa ndefu huwa kamili na zina mamlaka. Ni msingi kamili wa somo. Ni fursa ya kulinganisha taarifa za Biblia kwa waumini.
- C. Taarifa zinaweza kuchukuliwa kutoka katika andiko zaidi ya moja.
- 1. **Taarifa zinazo kamilisha.** Neno *kamilisha maana yake ni kitu kinachofanya kamili, timiza* au *fikisha katika utimilifu*. Kamilisha siyo kupongeza jambo ambalo ni la kusifu. Maandishi yanayothibitisha au kufanya kazi pamoja katika kueleza ukweli kwa ukamilifu ni taarifa zinazokamilisha.

# Mifano ya taarifa zinazokamilisha:

#### MFANO 1:

"Mimi ndimi mlango wa kondoo" - Yohana 10:7

"tumepata kwa njia ya Imani" - Warumi 5:2

"Sote tumepata njia ya kumkaribia katika Roho mmoja" -Waefeso 2:18

"Kupaingia pakatakatifu kwa damu ya Yesu" - Waebrania 10:19

#### MFANO 2:

"Mhudumu mwuaminifu wa Kristo" - Wakolosai 1:7

"Mimi Paulo nalikuwa mhudumu " – Wakolosai 1:23 (mhudumu wa Injili)

"Mhudumu wa kanisa" - Wakolosai 1:24-25

#### MFANO 3:

"utamlinda katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini:" - Isaya 26:3

"Na amani ya Mungu ipitayo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." - Wafilipi 4:7

2. **Kutofautisha Vifungu vya Maandiko.** Neno *tofautisha* lina maana *linganisha kwa kuchambua kisichofanana*. Maandishi yanayoonesha zaidi ya upande mmoja au tabia ya somo ni taarifa tofauti. Ni muhimu kuelewa kwamba maandishi haya *yanatofautiana* na siyo kwamba *yanapingana!* 

Mifano ya vifungu vya Maandiko vinavyotofautiana:

#### MFANO 1:

"Maana Mungu wetu ni moto ulao" - Waebrania 12:29

"Kwa maana Mungu ni upendo" - I Yohana 4:8

#### MFANO 2:

"acha sasa tuanguke mikononi kwa BWANA; kwa kuwa huruma zake ni za ajabu:" - 2 Samweli 24:4

"ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai."

- Ebr. 10:31

#### MFANO 3:

"Mimi Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu nawapatiliza wana maovu ya baba zao," - Kutoka 20:5 "Mwana hatauchukua uovu wa baba yake," - Ezekieli 18:20

3. **Vifungu vya Mandiko sambamba.** Neno sambamba maana yake *upande kwa upande, kuelekea upande mmoja, sawasawa au inayofanana.* Kulinganisha ni kuonyesha jinsi vitu vinavyofanana. Vifungu vya Maandiko ya neno moja kwa njia mbalimbali yanaweza kusemwa kwamba ni vifungu vya mandiko sambamba.

Mifano ya vifungu vya Maandiko sambamba:

#### MFANO 1:

Maneno "kama" katika sura ya kumi na moja ya kitabu cha Yohana yamesimama kama vilele vinavyofuatana mfululizo katika mlima mmoja. - Yohana 11:9, 10, 12, 21, 40

#### MFANO 2:

C.H. Spurgeon alihubiri kwa maneno "nimetenda dhambi":

- Farao aliyekuwa shupavu Kutoka 9:27
- Balaamu aliyekuwa kigeugeu Hesabu 22:34
- Mfalume Sauli mdhambi I Samweli 15:24
- Akani akajuta Yoshua 7:20 (samahani amekamatwa, lakini hakutubu)
- Yuda akaumia rohoni Mathayo 27:4
- Ayubu akashangazwa na uadilifu wa Mungu Ayubu 7:2
- Mwana mpotevu alitubu Luka 15:21

# III. Kufanyia kazi Kifungu cha Maandiko

# A. Hotuba ya kutumia kifungu cha Maandiko

- 1. **Migawanyo**. Maneno muhimu ndio yanayofanya sehemu za hotuba. Yafuatilie kwa umakini maneno yaliyoandikwa kipengele kwa kipengele. Maandishi hayo yanatenganishwa katika vifungu vinavyofaa kufanyia kazi, kwa ajili ya uchunguzi kamili. Maandishi hayo hayapasuliwi kama mtu anayevunja kwa nyundo kama mtoto anavyoweza kupasua saa. Maandishi hayo yanagawanywa kwa umakini wa
- mtengeneza saa.
- 2. **Mafanikio**. Mafanikio ya kuandika hotuba yanategemea uchaguzi wa maandishi. Maandishi ya aina fulani yanafaa zaidi kuliko mengine kwa ajili ya kazi ya hotuba. Maandishi mengine ni bora zaidi kwa ajili ya kupanga mada. Maandishi yanaweza kuwekwa katika njia mbalimbali.
- 3. **Uchambuzi**. Uchambuzi sahihi wa maandishi. Uchambuzi kutenganisha, au uvunjaji wa kitu chochote hadi kupata mtungamano wake; chambua chana katika vipande; kukagua kwa makini sehemu kwa sehemu. Webster.
- 4. **Lugha sahihi.** Kugawanya maandishi katika lugha yake sahihi. Kwa uwazi, kupata viungo vyake asilia katika maandishi. Tafsiri sahihi ya maneno ya maandishi. Maana yake katika lugha ya asili. (kitabu cha Strong kiitwacho Mzabibu) Tafakari ya taarifa kwa maneno yaliyoko ndani ya msitari. Kutafakari taarifa ya msitari ndani ya taarifa yote.

- 5. **Kutambua tabia** ya mafundisho ya namna hii. Inapaswa kuwa ya kawaida na rahisi kuijenga mtiririko wa wazo kwa wazo. Usilazimishe kugawanya mahali pasipofaa panapokaribia kuvunjika. Inapaswa kuwepo na maendeleo mazuri ya mawazo. Kila kipande kinapaswa kuipeleka mada hatua moja mbele kukaribia kilele. Siyo lazima kuyagawa maneno kama yanavyotokea ili mradi kunakupiga hatua katika somo lenyewe.
  - B. Hotuba ya kutumia kifungu cha Maandiko Ki Mada
- 1. **Migawanyo.** Ugawanyaji wa somo unafanywa kwa mada, lakini kwa kuzingatia andiko. Maandiko menyewe huonesha uwezekano wa asili wa somo. (kuzingatia andiko). Wazo lililopo katika mgawanyo linaelezwa kwa kutumia maneno yaliyotolewa katika mada. (Kuelezwa kwa mada). Wazo linakuwa na umuhimu kuliko maneno katika andiko.
- 2. **Mafanikio.** Mafanikio ya andiko la somo hutegemea ulivyooanisha muungano wa mambo mawili:
  - 1) <u>Uchambuzi sahihi</u> ili kuamua mgawanyo wa maandishi na,
  - 2) Mada katika mgawanyo inapaswa kuelezwa kwa <u>lugha sahihi inayoeleweka</u>. "mafanikio yanayotegemea muungano wa uchambuzi wa mawazo katika akili ya mhubiri" James Pattison.

Neno *usanisi* maana *ni mchanganyiko au kuweka pamoja; kuunganisha sehemu ili kupata kitu kimoja; kinyume cha uchambuzi ²,* tenganisha vipande vya taarifa kwa lengo la kuweka sehemu zilizochambuliwa kama zilivyokuwa mwanzoni. Kunapaswa kuwepo na uendelezaji wa wazo.

- 3. **Kutambua tabia.** Mfumo wa kuandika kwa mada huhakikisha uchangamfu na mchanganyiko wa maoni katika somo. Mhubiri anashikiliwa ndani ya maneno katika andiko njia inayohakikisha msingi imara wa Biblia lakini huruhusu pia uhuru wa kuwaza. Usikae usahau kwamba mamlaka ya mhubiri yanatoka katika lile Neno
  - C. Hotuba ya kifungu cha maandiko-kutumia kilichotolewa wazo
- 1. **Migawanyo.** Mada inapatikana katika maneno ya maandishi. Mgawanyo wa somo huamuliwa na maandishi. (Kutibu Maandishi). Mtiririko wa taarifa ndani ya maandishi huamuliwa na kilichoandikwa. Habari za ufahamu zinaweza kuwa katika maandishi na kinachoweza

\_

<sup>&</sup>lt;sup>2</sup> Ufafasnuzi unaopatikana katika kamusi ya Webster.

kuhitimishwa hutegemea kilichoandikwa. Taarifa za ufahamu kutoka katika kitabu cha Ufunuo 3:20 zinaweza kuwa:

Ufu. 3:20 - Tazama nasimama mlangoni, nabisha mtu akiisikia sauti yangu na skuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye na yeye pamoja nami.

- Kristo yuko nje lakini hajaliacha kanisa lake. Hajaliacha, lakini amesimama akibisha hodi "Tazama, nasimama mlangoni na kubisha hodi....."
- Kristo anaongea kitu ambacho kanisa linahitaji kusikia, lakini kwa ujumla halitasikiliza. Wamemfungia mlango kwa hiyo anatoa wito kwa mtu binafsi "...mtu akiisikia sauti yangu ..."
- Kristo aliwafunulia watu ukweli wa Mungu ambao utamfanya mtu binafsi kushinda na kupokea ile ahadi katika mstari wa 21. "... nami nitakula pamoja naye,..."
- Ufunuo 3:21 Yeye ashindaye, nitampa kuketi nami katika kiti cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. .
- 2. **Mafanikio**. Mafanikio ya maandishi ya somo la hotuba hutegemea uchaguzi wa taarifa ambazo zinakubali kuchambuliwa kwa njia hii. "taarifa hiyo inapaswa iwe mapendekezo yanaweza kupatikana ndani yake yenye kuelezeka; na somo linapaswa lihifadhi kwa uaminifu maana yake, na inapowezekana maneno yale yaliyoandikwa ."
- Pattison.

Maana yake inapaswa kuwa wazi, inayoelezeka na kueleweka kwa urahisi kwa waumini. Maana sahihi ya taarifa za Biblia siyo kitu cha kukisia bila ushahidi wenye maelezo. Maelezo yeyote mazuri hayatapingana na ukweli wowote wa Biblia katika mstari huo au mstari mwingine wa Maandiko. Maandishi ya maelezo yanapaswa kuwa ni ukamilisho wa wazo. Kwa lugha rahisi kila kilichomo katika maandishi kinapaswa kuwa cha maana na kinachoelezeka kuonesha nia ya taarifa hiyo.

Mafanikio mengi ya mfumo wa maandishi wa somo hutegemea uwezo wa akili ya mhubiri. Ni lazima mhubiri awe na uwezo wa kuonesha kiasi cha kutosha ukweli uliopo. Akili yenye uwezo wa kuchambua na kukubali ubishi ndio iliyobora kwa ajili ya mafundisho ya aina hii. Mafundisho ya namna hii huwa na mafanikio makubwa "kwa wakati mmoja huchambua, hupima, ni ya ubishi na kurudia rudia hali ambayo inavuta usikilizaji wenye heshima."- Pattison.

#### D. Hotuba ya kutumia mada

- 1. **Migawanyo.** Mafundisho ya somo hutegemea mada au kichwa cha habari zaidi kuliko maneno yaliyoko kwenye taarifa. Mada huonekana wazi zaidi katika mafundisho ya somo. Sehemu za somo hutengenezwa na mhubiri (jambo hili msingi wake ni mada.) Maandishi kwa asili yanapaswa kuonesha mada ijapokuwa mada inaweza kuchaguliwa kwanza. Njia inayotumika kuweka utaratibu wa maandishi itakuwa ni ya kurudia rudia kwa kuweka mkazo katika mada. Mafundisho ya somo ni lazima yaoneshe somo kwa ukamilifu.
- 2. **Faida** za mafundisho ya somo. Inaruhusu kusisitiza mpaka somo likamilike. Inarahisisha mada kufanyiwa uchambuzi wa kutosha. Inaiweka akili katika mapana ambayo picha nzima huonekana. Mafundisho ya somo huhamasisha kwa kiasi kukubwa kutafakari vizuri **BARAZA LOTE LA MUNGU**.

#### 3. Tabia zinazotofautisha:

#### a. **Inayoonekana**

Mafunzo kwa njia ya hotuba hutoa fursa ya kutumia michoro na hadithi.

#### b. Ya Msimu

Mafundisho ya somo huinua vilele vinavyofuatana hadi kufikia hatima yenye maelezo mazuri.

#### c. Hushawishi

Uwezekano wa kuwepo mabishano unapaswa kuwepo katika kila hotuba. Busara haitakiwi iachwe kwa ajili ya ubishi.

#### d. Endelevu

Mawazo yanaoneshwa, kufikiwa, na kufanyiwa marejeo. Matumizi ya kawaida yanatakiwa yapatikane katika kila somo.

4. **Mafanikio** Mafanikio ya mafunzo kwa njia ya hotuba hutegemea uwezo wa kusisitiza alionao mhubiri.

Anapaswa kuwa mwanafunzi wa Neno la Mungu na awe na uwezo wa kupangilia namna ya kuuonesha ukweli. Nguvu za somo hili zimo katika mada iliyoko mkononi. Mafundisho ya somo yanayokubalika ni yale yanayokamilisha maonesho ya mada ambapo kila upande wake unaangaliwa vizuri.

#### E. Hotuba ya Kufunua undani

Hotuba inayoweka ukweli hadharani ni ile yenye uchambuzi kamili wa maandishi. Somo la namna hii limefanyiwa kazi kwa kina katika **Mahubiri kitabu cha III** na haitashughulikiwa sasa.